IFIT

INSTITUTE FOR INTEGRATED TRANSITIONS

Makala ya Mjadala ya IFIT

Mei 2023

# Kanuni za Kwanza: Hitaji la Makubaliano Mapana Zaidi Kuhusu Misingi ya Utengano

*Mjadala kuhusu hatari za utengano ni wa kimataifa. Lakini hadi kutakapopatikana maafikiano zaidi kuhusu fasili yake ya kimsingi, masuluhisho yanayohitajika sana kwa utengano wa mifumo ya kijamii na kisiasa yatabaki kuwa ya dharura na yasiyokuzwa.*

Mwandishi ni **Mark Freeman**, Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa IFIT

Mnamo mwaka wa 1939, Winston Churchill aliripotiwa kufafanua nia ya kisiasa ya Urusi kuwa ni "kitendawili, kilichofumbwa kwa fumbo, ndani ya siri kuu." Mnamo mwaka wa 2023, usemi huu unaweza kuhusishwa na uelewa wetu wa pamoja wa neno "utengano".

Hakika, mada hii ni tata. Hata hivyo, wakati umefika wa kukabiliana kwa uthabiti zaidi na utata mwingi unaoendelea wa mada hii na kuanza kufikia uelewa wa kimsingi wa pamoja wa utengano. Manufaa yanaweza kuwa makubwa, yakiwezesha uboreshaji wa uwezo wa kutambua sababu na dalili za utengano zinazotegemea mahali, kubuni mikakati thabiti ya maonyo na ukabilianaji wa mapema, kupima athari za usuluhishi kwa usahihi zaidi, na kuepuka kuwakera washirika watarajiwa ambao wanapinga matumizi fulani ya neno hili.

Makala hii ya mjadala ina sehemu tatu kuu, na imekusudiwa kama hatua ya vitendo ya kutimiza malengo yanayohusika. Sehemu ya kwanza inazingatia kiwango cha mawazo, ikichunguza ukinzani unaoendelea katika uelewa wetu wa utengano na kutoa fasili "kuu" ambayo inaweza kuweka msingi wa siku zijazo. Sehemu ya pili inarejelea utafiti wa kimataifa wa mazoezi ya kuondoa utengano, na kazi ya nyanjani ya IFIT yenyewe, ili kuunda wigo wa suluhu ambao unalingana kwa upana na fasili kuu. Sehemu ya tatu inachunguza kwa ufupi athari za kutokuwepo kwa mtandao wowote uliopangwa wa kimataifa wa wasomi na watendaji wanaoshirikiana kukabiliana na utengano, na inaangazia uwezekano wa kuanzisha "tasnia" ya utengano.

Ingawa tatizo la utengano halikaribiani hata kidogo na vita vya wenyewe kwa wenyewe, ubabe, mauaji ya halaiki na maovu mengine kama hayo, linaweza – likipuuzwa – kuwa kitangulizi na kichochezi cha mambo haya. Linaweza kurejelewa

kama tatizo kuu: tatizo linalofanya suluhisho la matatizo mengine yote kuwa gumu zaidi. Utengano unaweza kuongezeka polepole hadi kutishia kila kitu – kuanzia jamii bora yenye ustahimilivu, hadi shughuli za siasa na utungaji sheria wa kawaida, hadi matarajio ya kuishi pamoja kwa amani na uhuru wa kimsingi.

## SEHEMU YA KWANZA: FASILI YA DHANA YA UTENGANO

Sehemu ya kwanza ya makala hili inatanguliza msururu wa utata wa jinsi utengano unavyoeleweka, inajadili njia za kutatua utata huu, na kupendekeza fasili ya utengano inayozingatia sifa zake za kimsingi.

### 1. Utata wa fasili

Katika utafiti huu, usaili pamoja na vikao vilivyofanywa katika miezi kumi na minane ya kwanza ya **Mpango wa Kimataifa wa Kukabiliana na Utengano** uliondaliwa na IFIT na Ford Foundation, aina sita za utata na tofauti za kidhana zilijitokeza mara nyingi. Katika kuelezea hoja hizi, lengo ni kuangazia baadhi ya mafumbo ya kifasili ambayo yanahitaji kutatuliwa ili kuweza kukabiliana, kuzuia na kutathmini utengano kwa ufanisi zaidi.

Aina hizi za utata ni sahili mno, lakini hupuuzwa kutokana na usahili wake, hasa kutokana na wingi wa vivumishi vinavyoambatishwa mara kwa mara na neno utengano (k.m., kihisia, kiitikadi, kuilinganifu, kiukosefu wa ulinganifu, kisiasa, kijamii, kikabila, kidini, kirangi, kiusomi, kiwingi, kiuharibifu, kisumishaji, kiusalama na kadhalika).

#### Kudumu dhidi ya Kutodumu

Je, utengano ni jambo linalotokea na kutoweka, ikimaanisha kuwa mifumo ya kisiasa na jamii inaweza kukoma kuwa na utengano? Au ni jambo la kudumu, kwa maana kuwa mifumo ya kisiasa na jamii huwa na utengano daima kwa kadiri fulani? Mtu anaweza kuchukulia kuwa swali hili la kimsingi lilitatuliwa zamani, lakini sivyo. Kwa kundi moja kubwa la wataalam, utengano ni hali ambayo watu wanaweza kuingia na kutoka. Kwa kundi lingine – ikiwa ni pamoja na waandishi wa kazi kubwa ya ulinganishaji violezo na **kutathmini utengano** – ni jambo ambalo linaweza kuzidi au kupungua lakini, kama migogoro, kamwe haliwezi kuepukika.

#### Hasi dhidi ya Chanya

Utata wa pili, ambao unahusiana na wa kwanza kwa kiasi fulani, unachunguza iwapo utengano daima huathiri mifumo ya kijamii na kisiasa, au wakati mwingine unaweza kuwa "salama". Watetezi wa mtazamo wa kwanza wanasema kuwa utengano ni hali inayopaswa kuzuiwa au kukabiliwa. Kinyume chake, kuna wengi ambao wanaamini utengano unaweza kustahimiliwa au hauna madhara au manufaa, na unasababisha

wasiwasi tu ukizidi kiwango fulani na kuleta “uharibifu”, “ukali” au “madhara”. Mtazamo mwingine wa dhana hii ni kwamba utengano ni jambo chanya, kama inavyoonekana katika ushauri wa Saul Alinsky unaotajwa mara kwa mara na wapenda maendeleo kwamba **“ili kuratibu, lazima kwanza utenganishe”**. Wazo linalohusika ni kwamba kwa harakati kubwa ambazo zinahitaji uhamasishaji mkubwa wa washirika, ni mkakati mzuri kukuza utengano. Jambo lisiloeleweka zaidi ni ikiwa waitifaki wa mtazamo wa Alinsky wanapendekeza mbinu (na matokeo) sawa wanapoichukulia harakati inayohusika kuwa haramu.

## Pande mbili dhidi ya Pande nyingi

Utata mwingine unaojitokeza sana katika mijadala kuhusu utengano wa mifumo ya kijamii na kisiasa hujikita katika dhana ambayo ni ya kimsingi pia: iwapo utengano daima huhusisha pande mbili au unaweza kuhusisha pande nyingi. Muundo wa pande mbili pekee – ambao mara nyingi hudokezwa bila kufumbuliwa wazi – unasema kuwa utengano hutokea tu kati ya ncha au mihimili miwili, sawa na asili ya istilahi hii inavyopendekeza. Kinyume chake, muundo wa pande nyingi – mtazamo unaohusishwa zaidi na hali tete na aina za “kimbari” za utengano – unasema wazi kuwa utengano unaweza kutokea katika mihimili kadhaa. Ni ajabu kwamba hoja ya kimsingi kama hiyo tayari haijadiliwi katika mada wazi na iliyoenea baina ya wataalam.

## Mlalo dhidi ya Wima

Utata wa nne mkuu unahusu mwelekeo wa utengano na, isitoshe, nafasi na nguvu linganifu za “pande” zinazohusika. Kwa wasomi na wataalamu wengi, utengano unaonekana kuashiria mienendo ambayo kimsingi ni ya mlalo na inayoanzia katikati, inayohusisha uvunjaji unaoendelea kukua kati ya pande za ukubwa au nguvu zinazolingana. Hata hivyo, utengano pia wakati mwingine hutumiwa kueleza mienendo wima na linganifu ambapo upande wenye nguvu (k.m., kundi kubwa la kijamii au serikali kuu ya kimabavu) huwa na uhasama mkubwa dhidi ya, na kuweza kutawala upande mdogo na usio na uhasama mkubwa ikilinganishwa.

## Razini dhidi ya Kihisia

Sehemu ya tano ya utata katika maandishi na utendaji inahusiana na iwapo utengano ni hali ambayo “hisia” (yaani, mhemko) hushinda au kudhoofisha kwa kiasi kikubwa uwazi wa mtu binafsi na wa kikundi wa kushawishi kuhusu masimulizi mbadala na ukweli kinzani. Kwa wengine, hisia ni kiini cha dhana (yaani, watu walioathiriwa na utengano ni watu wanaotawaliwa zaidi na hisia). Kwa wengine, utengano ni kitambulisho ambacho kinaweza pia kutumiwa kufafanua mizozo baina ya vikundi vinavyozozana, mizozo ambayo imejikita kwenye misingi ya kimawazo. Mizozo kama hii ndiyo watetezi wa amani huiita aina ya “nzuri” mizozo.

### Kubwa dhidi ya Ndogo

Utata wa sita kuhusu dhana ya utengano unahusu kiwango cha chini kabisa ambacho neno hili linafaa kutumika kutaja matatizo katika mifumo ya kijamii na kisiasa. Mara nyingi, istilahi hii huhusishwa na migawanywo ambayo imefikia kiwango kikubwa cha kijamii na kisiasa na kuwa tatizo kubwa la umma. Hata hivyo, kuna baadhi ya wale wanaotumia istilahi ya utengano kufafanua mizozo midogo baina ya vikundi au masuala ya jamii ndogo, hata wakati mizozo hii haina misukumo au athari za kiwango kikubwa. Baadhi ya utata huu unaweza kusababishwa na njia ya kawaida ambapo kitenzi “kutenga” huhusishwa na nomino “utengano”, kiasi kwamba kauli au vitendo vya utengano huchukuliwa kuakisi uwepo wa hali ya utengano, hata kama kuna migongano ya hapa na pale.

**Aina sita maarufu za utata za jinsi utengano unavyoeleweka**

1. Kudumu dhidi ya Kutodumu
2. Hasi dhidi ya Chanya
3. Pande mbili dhidi ya Pande nyingi
4. Mlalo dhidi ya Wima
5. Razini dhidi ya Kihisia
6. Kubwa dhidi ya Ndogo

## 2. Kuukabili utata

Iwapo utengano haungekuwa na hatari yoyote, utata unaozunguka fasili yake haungekuwa chanzo cha wasiwasi wowote. Tungeweza kuzijadili kwa utulivu au kuzipuuza fasili hizi. Hata hivyo, utengano ni tatizo linaloongezeka kwa kasi kwa makundi mengi katika mifumo tofauti ya kijamii na kisiasa. Kiasi cha taarifa zilizoandikwa duniani kote kuhusu utengano ni kikubwa mno, na kinaongezeka kwa kasi mno hivi kwamba haiwezekani kudai vinginevyo.

Aidha, ili kuwa na ufanisi zaidi katika kuchunguza, kuzuia, kukabili na kuutathmini utengano, kuna haja kubwa ya usahihi zaidi katika jinsi tunavyoelewa na kutumia istilahi hii. Hasa, kunahitaji kuwa na juhudi za makusudi za kufikia maelewano zaidi hatua kwa hatua kuhusu sifa ndogo zaidi za utengano na kutafakari kwa kina kuhusu wingi wa vivumishi vinavyofaa ambavyo vinatumika sasa, ambavyo vinatatiza badala ya kuwezesha udhahiri wa kifasili.

Kwa mfano, zingatia ukosefu wa kijumla wa utata wa neno linganifu kama “ufarakano”. Tofauti na utengano, hakuna utata kuhusu kama ufarakano ni hasi au chanya kwa mifumo ya kijamii na kisiasa; ni dhahiri kwamba ni jambo hasi (au bovu) kwa fasili yoyote ile. Pia, ni wazi kutokana na mzizi wa neno “farakana” kwamba ufarakano hudhihirisha jinsi hisia zinavyotawala mawazo (“mshikamano wa nia finyu”: Oxford). Kipimo cha chini pia kinaonekana, kwa kuzingatia mzizi wa neno “faraka”, ambalo ni kundi ndogo linaloashiria ukubwa muhimu.

Jambo linalojitokeza nii kwamba ufarakano ni dhana ambayo imefikia ukomavu wa kidhana na kifasili. Katika ufarakano, vivumishi vya sifa kama vile “mbovu” na “kihisia” ni dhahiri. Tunapotumia neno hili, kuna uelewa wa kjimsingi ambao

unafahamika kwa kila mtu. Vivumishi vyovyote vinavyostahiki tunavyoweza kuongeza ("kisiasa, kikabila au kidini": Oxford) hutumika tu kuleta uwazi au usahihi zaidi kwa neno msingi, badala ya kuimarisha utata uliopo tayari, au kuanzisha utata mpya.

Tukilinganisha na utengano, bado tuko katika hatua ya kwanza ya kuikuza dhana hii. Tunairuhusu dhana hii ichukuliwe kuwa vitu vyote: chanya na hasi; razini na kihisia; mlalo na wima; ndogo na kubwa; na kadhalika.

Utata mkubwa kiasi hiki, ukiruhusiwa kuendelea, sio tofauti zenye manufaa. Kwa jumla, ni vyanzo vya kutoelewana, ambapo, kwa mfano, utengano unaweza kulinganishwa na kila kitu kuanzia kukabiliana na ukandamizaji, hadi ushindani kati ya koo za kifamilia au makampuni yanayoshindana, hadi mzozo mkubwa wa kisera kati ya vyama vya siasa katika demokrasia ya wingi.

Yamkini, hakuna hata mojawapo ya mifano hii inapaswa kufafanuliwa kama utengano. Hata hivyo, wingi wa utata ambao tumeruhusu kuwepo, na kisha kuimarishwa kupitia maelfu ya vivumishi vinavyostahiki, umesababisha kuruhusiwa kwa ulinganisho huo wenye kutiliwa shaka.

## 3. Kuelekea msingi mmoja

Haitawezekana kuafikiana kabisa kuhusu fasili ya istilahi utengano. Azma ya makala hii ni rahisi mno: kuibua mjadala uliopangwa miongoni mwa wasomi na watendaji ambao, baada ya muda mrefu, unaweza kusaidia kusababisha uelewa mmoja wa kimsingi wa utengano, sawa na uwazi wa neno kama ufarakano. Kutokana na uelewa huu, kutakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa nchini na kimataifa kwa ajili ya onyo la mapema, ushirikiano wa kimkakati, mwitikio madhubuti na ukadiriaji athari.

Ili kufanya hivyo, makala hii inatumia **mbinu ya sifa kuu** kupata fasili iliyopendekezwa ya utengano. Mbinu hii wakati mwingine hutumiwa katika sayansi asilia, kwani inasaidia kupanga mawazo changamano sana na kujumuisha matumizi ya kawaida na maana fiche za neno linaloainishwa.

Kabla ya kutumia mbinu hii, hoja tatu zinahitaji kutajwa. Kwanza, fasili ya utengano iliyo katika makala hii inazingatia kwa makusudi asili nyingi za kimantiki za neno hili, ambazo zilianzia angalau Ugiriki ya kale (dhana ya **mkatizo** ni muhimu hasa). Dhana za kijamii na kisiasa za utengano tangu katikati ya karne ya ishirini zinaonyesha uakisi mkubwa nadharia hii ya kale na zimeathiriwa kwa muda mrefu na nyanja nyingine nyingi za maarifa, zikiwemo saikolojia ya kijamii na uchumi wa kitabia. Kinyume na hili, maana ya utengano katika **fizikia**, ambayo huzingatia mitetemo ya vekta ya umeme ya mawimbi ya mwanga, imekuwa na ushawishi mdogo zaidi (jambo linaloshangaza).

Hoja ya pili inahusu etimolojia ya neno utengano, ambayo inajumuisha angalau dhana mbili muhimu: Dhana ya ncha inaeleweka zaidi na kutajwa kwa maneno ya pande mbili katika kurejelea mifumo ya kijamii na kisiasa (yaani, inahusisha ncha mbili zinazoungana kujenga uwili). Kifasili, ncha humaanisha umbali wa

kiulinganisho, kinyume na ukaribu wa kiulinganisho. Nacho kitenzi cha tenganisha, kawaida huashiria ukubwa. Mtu hawezi kamwe, kwa mfano, kutumia neno hili kueleza hali ya kiakili au kiroho isiyoegemea upande wowote au ya kutojali (yaani, mpiga kura aliyetengwa si mpiga kura mwenye amani). Mwishowe, maneno haya yanapounganishwa, hali ya utofauti inadokezwa kimantiki. Watu waliotengwa huwa katika ncha, hivi kwamba kichochezi kinachosababisha tatizo huongeza, wala si kupunguza, umbali kati ya ncha hizi mbili.

Jambo la tatu linahusu umuhimu wa visawe na maana ambayo inaweza kutolewa kutoka kwake. Kwa mfano, wakati wa kueleza utengano wa mifumo tofauti ya kijamii na kisiasa, istilahi kama vile migogoro, migawanyiko, ukabila, ufarakano, misimamo mikali na itikadi kali ni miongoni mwa vibadala au milinganisho inayotumika sana. Haya si maneno chanya wala yasiyoendelea upande wowote; badala yake, yanaashiria matukio hasi. Kinyume chake, maneno kama vile ukandamizaji, uchokozi au uonevu – ambayo pia huashiria matukio hasi lakini ambayo yanahusiana na hoja wima zaidi na zisizolingana – hayatumiki sana kama visawe vya utengano. Vilevile, maneno kama vile ushindani, mavurugano na upinzani – ambayo yanahusisha mienendo ya mlalo na linganifu zaidi, lakini yanaashiria uzito au hatari kwa kiasi kidogo zaidi – ni nadra kulinganishwa na utengano. Machaguo haya ya maneno ni ishara ya jinsi utengano unavyoeleweka kwa upana.

## 4. Fasili inayopendekezwa

Ingawa huenda tukazua ubishi licha ya lengo la kukuza mjadala uliopangwa, makala hii inatoa fasili ya utengano ifuatayo:

> **Utengano:** mgawanyiko au mzozo wazi kati ya makundi makubwa katika jamii au mfumo wa kisiasa na unaoashiriwa na mikusanyiko na misimamo mikali ya kimaoni na kiimani katika ncha mbili kinzani na za mbali.

Fasili hii inayopendekezwa inatokana na nguzo nane za utengano, ambazo zinapaswa kusomwa kama kitu kizima kilichounganishwa, ambapo kubadilisha nguzo moja kunaweza kusababisha mabadiliko katika nguzo nyinginezo.

### Umbali

Nguzo hii inatokana na dhana msingi ya ncha na inaakisiwa katika matumizi mengi. Kwa asili yake, ncha huwepo katika umbali mkubwa kati ya moja na nyingine, iwe umbali huo ni halisi, kiitikadi au kihisia. Ncha zina sifa za ukosefu wa ukaribu.

### Uwili

Tofauti na misimamo mikali, itikadi kali, ufarakano au ukabila, utengano kawaida hueleweka kuhusisha uhusiano baina ya ncha au peo mbili. Migogoro inapohusisha pande nyingi – jambo linalotokea sana – istilahi nyingine huhitaji kutumiwa (k.m., mgawanyiko, ugomvi, mgogoro), wala sio kivumishi kipya mwafaka.

### Ukubwa muhimu

Kiasili, ncha huwa aina fulani ya usawa baina ya moja na nyingine, kama ncha mbili za sumaku au mhimili. Kama ilivyotabiriwa, hali hii haijumuishi matumizi ya neno utengano kueleza hali ambayo eneo la kati ni kubwa kuliko ncha. Lebo ya utengano inaeleweka tu ikiwa kuna ukubwa muhimu, iwe kihalisi au kidhana, katika kila ncha na sehemu ndogo katikati.

### Kuanzia katikati

Nguzo hii hutumiwa sana, na pia inatiririka kimantiki kuanzia makutano ya mizizi ya maneno “tengwa” na “ncha”. Watu waliotengwa ambao wapo kwenye ncha tofauti huwa na mtindo wa kusonga mbali na, wala si kuelekea kwenye ncha kinzani. Kutafuta njia za kufikia utambuzi wa pamoja, kuepuka misururu ya mrejesho haribifu, na kupanua kile ambacho wapatanishi hukiita **“eneo la uwezekano wa makubaliano”** ni changamoto za kimsingi za utengano.

### Kimlalo

Utengano kimsingi ni tatizo la uhusiano ambapo, kimuundo, hali huwa ya kimlalo kuliko ilivyo ya kiwima. Kwa hivyo, suluhu hudhamiria zaidi kurekebisha uhusiano kuliko kujilinda dhidi ya aina ya mashambulizi ya njia moja ambayo, kwa mfano, mfumo wa Nazi nchini Ujerumani au ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini ni maarufu. Utengano si hadithi ya Daudi dhidi ya Goliathi; ni hadithi ya mzozo kati ya makundi mawili yenye ukubwa sawa (iwe ni katika mamlaka, idadi au ushawishi).

### Kutodumu

Muhtasari wa nguzo kuu ya kuanzia katikati (ambayo ni dhana ya mwendo) ni kwamba utengano ni hali ambayo watu wanaweza kuingia na kutoka ndani yake. Hoja ni kwamba, mwendo kati ya ncha zote unapoelekea katikati kwa muda mrefu, hoja ya utengano basi haina msingi. Hoja hiyo pia inatumika kwa neno mizizi la “ncha”: sehemu ya katikati inapopanuka na kuwa kubwa kuliko ncha, haiwezekani kimantiki kusema kuna ncha, na hivyo hakuna utengano.

### Tishio

Sio kila mzozo mkali unaweza kuainishwa kuwa utengano. FC Barcelona dhidi ya Real Madrid sio mfano wa utengano; mashabiki wao ni washiriki tu wa ushindani. Magari dhidi ya watembea miguu sio mfano wa utengano; watetezi wao wako katika pande tofauti za mzozo wa kisera. Utengano huhusisha hoja kubwa zinazohusisha vitisho wazi dhidi ya amani ya mfumo wa kijamii au kisiasa. Kwa chochote kisichotimiza kadirio hili, kuna maneno bora ya kutumia.

### Utofauti

Nguzo hii mahususi inatokana kimantiki na nguzo nyingine nyingi, na inapishana moja kwa moja na matukio kama vile ukabila na ufarakano na msisitizo wake kuhusu uadui kati ya makabila na mafarakano, mtawalia. Katika utengano, mambo si tofauti.

Katika hali ya utengano, hisia ni za kawaida. Mitazamo hubadilika kuwa mikali, utata hupungua, imani huchukua nafasi ya mawazo, na mchanganyiko wa kuungana mikono ndani ya kikundi na kuwalaumu watu wa nje ya kikundi hushamiri.

**Nguzo nane za utengano**

1. Umbali kwenda Sol:
2. Uwili
3. Ukubwa muhimu
4. Kuanzia katikati
5. Kimlalo
6. Kutodumu
7. Tishio
8. Utofauti

Kama ilivyosisitizwa awali, fasili hii haikusudiwi kuhitimisha mjadala bali ni kuchochea mijadala iliyopangwa zaidi kuhusu uelewa wetu wa pamoja kuhusu utengano ni nini na si nini. Mchakato huo utahitaji muda, pamoja na ufahamu uliotajwa wa vivumishi zaidi vinavyostahiki.

Hatimaye, itawezekana kuzungumzia utengano kwa njia isiyo tata ambayo watu huzungumzia ufarakano, ambayo vivumishi vinavyostahiki ambavyo ni finyu na chache kwa sababu fasili ya kimsingi imebainika. Kinachopaswa kujitokeza, hatimaye, sio kikomo cha kidhana ambacho huondoa utofauti na unymbufu wa jinsi utengano unavyoeleweka, badli msingi wa kidhana unaowezesha usahihi zaidi.

## SEHEMU YA PILI: WIGO WA SULUHISHO LA UTENGANO

Sehemu ya pili ya makala hii inawasilisha utangulizi wa wigo wenye sehemu tatu za suluhu la tatizo la utengano katika mifumo ya kijamii na kisiasa. Inajumuisha tafakari zinazopanua baadhi ya maswali ya kidhana na kiutendaji yaliyoibuliwa katika uchanganuzi uliotangulia. Baada ya muda, toleo la kwanza la wigo huu wa suluhu linaweza kuboreshwa na kuimarishwa sambamba na ukuzaji wa maafikiano zaidi kuhusu sifa zinazobainisha utengano wenyewe.

### 1. Tathmini ya muktadha

Mjadala wenye tija wa suluhu la tatizo lolote la kijamii au kisiasa, lakini hasa lililo tata kama utengano, unawezekana zaidi kunapokuwa na maafikiano ya kimsingi kuhusu asili ya tatizo lenyewe. Kwa hivyo, uelewa mpana ulioshirikiwa na wahusika wote wa hoja hiyo ni muhimu. Hata hivyo, mtu lazima achambue ukweli kila wakati ili kubaini kama lebo husika inafaa.


Hatua hii sio ya kielimu. Utambuzi sahihi wa hali ni sharti linalopaswa kutimizwa ili kuunda mkakati wowote mzuri.

Kwa mfano, utambuzi ambao unategemea sana watendaji, mitandao, maarifa na uongozi wa "nje" badala ya wa "ndani" una uwezekano mkubwa sana wa kukosa lengo. Kinachoweza kuonekana kama utengano kutoka nje kinaweza kuwa kitu tofauti sana mtu anapokichunguza – na kukipitia mwenye – akiwa ndani.

Hata hivyo, kama kawaida, maelezo ya kina ni tata kuliko inavyoonekana. Ufafanuzi, miongozo, visanduku vya zana na orodha hakiki mwishowe hazina thamani ikiwa uchanganuzi pembuzi unaohusika una dosari kubwa. Hii inajumuisha usahihi kuhusu sababu kuu mahususi za muktadha, vitendaji, vichochezi, dalili na matokeo ya utengano. Tathmini ya ubora – inayosasishwa mara nyingi inavyohitajika – ni muhimu sana.

## 2. Kielelezo cha wigo wa suluhisho

Kupitia Mpango wa Kimataifa wa Kukabiliana na Utengano, juhudi zilifanywa kuainisha kimataifa, mashirika na miradi yote mikuu ambayo ilikuwa na nia wazi ya kuzuia au kukabiliana na utengano. Taswira wazi ilijitokeza kupitia zoezi hilo. Idadi kubwa ya mikakati na suluhu zilizojaribiwa ziliainishwa katika makundi matatu, kama inavyoonyeshwa kwenye kelelezo cha Venn hapa chini. Migao ya mlinganisho inapatikana katika baadhi ya maandashi ya hivi majuzi kuhusu utengano.




Kwa kuzingatia nguzo za utengano, sehemu isiyoshangaza sana katika kielelezo cha Venn ni "juhudi za ufikiaji na mazungumzo". Wakati kuna hatari ya mzozo au ikiwa mzozo utatokea kati ya makundi makubwa ambayo yanaainishwa na mkusanyiko wa maoni na imani katika misimamo kinzani, mazungumzo ni zana inayoeleweka kwa wale wanaotaka kuzuia au kupunguza utengano. Ni sawa na mtazamo wa mlinda amani na, kwa hivyo, mbinu na mikakati mingi inahusiana na nyanja za ulinzi wa amani na utatuzi wa migogoro.

Aina ya pili, "usuluhishi halisi na simulizi", pia inaambatana na nguzo za utengano. Wakati kuna ukuzaji wa maoni makali na utofauti kwa kiwango kikubwa, ni mantiki kwamba ufafanuzi wa uhalisi na mabadiliko ya simulizi yanaeleweka kama sehemu muhimu za suluhisho. Hizi ndizo hatua za ukweli na upatanisho na, kwa hivyo, mikakati mingi inatukumbusha tasnia ya haki ya mpito.

Aina ya tatu ni pana zaidi inayohusiana na mabadiliko ya mfumo ikolojia ambamo utengano unastawi au kupungua: Wazo ni kwamba utengano hautokei kiholela, bali ni matokeo ya hatua zinazochukuliwa katika mazingira ambayo hutoa mchanganyiko wa vivutio na vizuizi kwa aina fulani za tabia. Vigezo vingine vitabadilika kwa ugumu na polepole (k.m., jiografia, demografia, utamaduni wa kisiasa, viwango vya kusoma na kuandika) ilhali vingine vitakuwa rahisi zaidi ikilinganishwa (k.m., taasisi, sheria na

sera). Mabadiliko ya aina zote mbili za vigezo yataleta mabadiliko ya tabia miongoni mwa watendaji wakuu – kwa mfano, kuwashinikiza ili wafanye ushirikiano na ustahimilivu mkubwa au mdogo zaidi.

Uchunguzi zaidi unahitajika. Kwanza, chaguo la mchoro wa Venn ni kutokana na ukweli kwamba aina tatu za suluhu wakati mwingine hupishana. Kwa mfano, mchakato wa mazungumzo unaweza kulenga kubadilisha mazingira ya usimulizi ambayo yanazuia mageuzi ya kimuundo yanayohitajika. Aina zinaweza kuimarisha pande zote.

Pili, dhana mtambuka inaunganisha aina tatu, ambazo ni, kwamba usuluhishi wenye mafanikio unahitaji kujenga miungano, uchanganuzi wa kisiasa, uundaji wa mikakati na aina nyinginezo za shirika lenye malengo. Ingawa hakuna kati ya hizi ambayo ni aina ya suluhisho kivyake, kila mojawapo inaweza kuwa kiungo muhimu cha kimbinu kwa ajili ya mafanikio kwa kiwango kikubwa katika aina tatu za usuluhishaji.

Tatu, wigo wa suluhisho uliowasilishwa hapa juu si wa kina wala hautoi maelekezo (k.m., dini na michezo zinaweza kutumika kwa njia zinazolengwa kuondoa utengano). Badala yake, inakusudiwa kama njia ya kueleza viwango vikuu vya shughuli za mashirika na miradi iliyotambuliwa kupitia Mpango wa Kimataifa wa Kukabiliana na Utengano kama inavyofanya kazi kwa uwazi na kwa makusudi kukabiliana na utengano katika sehemu mbalimbali za dunia.

Jambo la mwisho ni kwamba baadhi ya vitendo vinavyohusiana na utengano vinaweza, kwa sababu mbalimbali, kupuuza lebo. Kwa mfano, kampeni kubwa ya kijamii kupinga kiongozi wa kimabavu ambaye amechochea waziwazi hali ya utengano wa kimbari, kisiasa au kidini huenda isifanywe chini ya mpango wa kukabiliana na utengano. Hiyo ni kwa sababu, kwa kawaida, lengo kuu na muundo sambamba katika matukio kama haya si kukomesha utengano bali kumkomesha mhalifu. Ingawa kufikia lengo hilo kunaweza kusaidia kupunguza utengano, ni athari ya pili badala ya nia msingi.

## 3. Maswali ya muundo wa usuluhishaji

Umuhimu wa tathmini ya muktadha umesisitizwa, na wigo wa usuluhishaji wa sehemu tatu umeanzishwa. Sehemu hii inachanganya vipengele hivi viwili kwa kuangalia ushawishi wa masharti ya kuanzia kwenye muundo wa usuluhishaji.

Angalau kanuni mbili kuu zinastahili kutajwa. Kwanza, jinsi utengano ulivyo mkali, ndivyo wigo mdogo uliopo wa mageuzi ya kimuundo (k.m., kwa sababu kuunda miungano ya vikundi mtambuka ni kazi ngumu zaidi), masimulizi mbadala yana athari ndogo zaidi na matokeo ya kutafuta ukweli bila upendeleo (k.m., kwa sababu ushikiliaji misimamo mikali na kurahisisha maoni na imani tayari umefunga akili za watu), na umakini wa ndani ya kikundi wa mazungumzo unaendelea kuwa muhimu zaidi (k.m., kwa sababu hakuna kikundi cha nje kinachokubaliwa na upande ule mwingine). Pili, kadiri mfumo wa kisiasa unavyozidi kuwa wa kimabavu, ndivyo kunavyokuwa na haja zaidi ya miungano ya makundi mbalimbali (k.m., kutetea

mageuzi ya kimuundo yaliyopitishwa kidemokrasia) lakini kuna nafasi ndogo zaidi ya kisiasa ya kujenga imani ya nje ya kundi (k.m., kwa sababu ya ukandamizaji) au ya kuripoti kwa njia huru na kuunganisha simulizi (k.m., kwa sababu ya ukandamizaji na udhibiti wa serikali dhidi ya vyombo vya habari).

Kwa kawaida, kuna masharti mengine mengi ya kuanzia yapaswayo kutathminiwa kabla ya kuandaa mwitikio wowote wa kimkakati. Hayo ni pamoja na maswali ya kimsingi kuhusu nani ametengwa na kwa nini, na kuhusu fursa zozote za kuzuia au kupunguza utengano (k.m., mishtuko ya nje au kuanzishwa kwa mazungumzo ya amani au mpito wa kisiasa). Lakini mara tu utambuzi thabiti na unaoongozwa kutoka ndani ukitayarishwa, aina tano za vigezo vinavyoweza kuunganishwa vinaweza kutumika kujenga muundo wa usuluhishi:

**Vigezo vitano vya usuluhishi**

1. Uzingatiaji wa ndani ya kundi dhidi ya nje ya kundi
2. Mtazamo wa ushirikiano dhidi ya makabiliano
3. *Malengo* ya muda mfupi dhidi ya malengo ya muda mrefu
4. *Kiwango* kidogo dhidi ya wastani dhidi ya kikubwa
5. *Wigo* wa mtaani dhidi ya kitaifa dhidi ya eneo dhidi ya kimataifa

**Muundo wa usuluhishi katika aina ya juhudi za mawasiliano na mazungumzo unaweza kuzingatia vigezo hivi vitano kwa njia nyingi. Kwa mfano:**

- usuluhishi wa ndani ya kikundi unaweza kujumuisha kuwasiliana na watu wa ndani wenye ushawishi ili kusaidia kuondoa misimamo mikali ya kikundi, nao usuluhishi wa nje ya kikundi unaweza kuhusisha kuwasiliana kwa siri na watu wa nje wenye misimamo isiyo mikali;
- mbinu ya ushirika inaweza kujumuisha hatua za upande mmoja za kujenga imani, nayo mbinu ya makabiliano inaweza kuhusisha ukosoaji hadharani wa wavurugaji wa mazungumzo yanayoendelea;
- lengo la muda mfupi linaweza kuwa kukubaliana kuhusu muundo wa mazungumzo rasmi, nalo lengo la muda mrefu linaweza kuwa kufikia makubaliano ya hatima yenye ufanisi;
- usuluhishi wa kiwango kidogo unaweza kulenga usitishaji makabiliano wa muda mfupi, nao usuluhishi wastani au mkubwa unaweza kulenga kutumia mazungumzo kutatua baadhi ya vyanzo vikuu vya utengano; na
- kwa mujibu wa upeo wa kijiografia, safu mbalimbali za nyenzo za mazungumzo ya mtaani, kitaifa, kikanda na kimataifa zinaweza kuhitajika ili kupunguza utengano baada ya mzozo unaohusu matumizi ya silaha baina ya mataifa yanayopakana, na yenye watu wa mataifa mengi.

**Kuhusu usuluhishi halisi na simulizi:**

- mwelekeo wa ndani ya kikundi unaweza kuhusisha juhudi za kubadilisha simulizi zinazosababisha mgawanyiko au kuvuruga juhudi za mitandao ya kijamii, ilhali mwelekeo wa nje ya kikundi unaweza kuelekezwa kwenye ufafanuzi jarabati wa historia zinazozozaniwa;
- mbinu ya ushirika inaweza kujumuisha mazoezi ya "mstakabali mbadala", ilhali mbinu ya makabiliano inaweza kuhusisha mashtaka ya kukabiliana na taarifa potofu/za uongo;
- lengo la muda mfupi linaweza kuwa kutoa mafunzo kwa wanahabari na majaji kuwawezesha kugundua upendeleo fiche, nalo lengo la muda mrefu linaweza kuwa kubadilisha simulizi mbaya;
- usuluhishi mdogo unaweza kuwa wa muundo wa kura ya maoni ya umma kuhusu suala lenye utata wa umma, nao usuluhishi wa kati au mkubwa unaweza kuhusisha uundaji wa tume ya ukweli na maridhiano "kupunguza kiwango cha uwongo unaokubalika" au utengenezaji msururu wa filamu ili kukuza kaida za amani za kijamii; na
- katika upeo wa kijiografia, mseto wa hatua za mtaa, kitaifa na kimataifa unaweza kuhitajika ili kushughulikia simulizi na desturi zilizokita mizizi, kwa mfano kuhusu utengano wa Kiislamu na kidunia katika mataifa ya Kiarabu.

**Kuhusu mabadiliko ya kimfumo:**

- mtazamo wa ndani ya kikundi unaweza kuhusisha uimarishaji wa demokrasia ya ndani ya chama kimoja cha siasa, ilhali mtazamo wa nje ya kundi unaweza kuhitaji kubadilisha kanuni ili kuchochea ushirikiano kati ya wahusika mbalimbali;
- mtazamo wa makabiliano unaweza kujumuisha usuluhishi wa kubadilisha sheria za mali zinazochochea utengano, ilhali mbinu ya ushirikiano inaweza kuhusisha kuanzishwa kwa bunge la wananchi kushughulikia suala la sera lililoshikamana;
- lengo la muda mfupi linaweza kujumuisha usaidizi wa kifedha wa muda mfupi kwa kikundi cha watu wachache maskini waliodhulumiwa, nalo lengo la muda mrefu linaweza kuzingatia sera za kurekebisha ukosefu wa usawa wa kiupana uliojikita au kubadilisha tamaduni za kisiasa za "mshindi huchukua mamlaka yote";
- usuluhishi mdogo unaweza kulenga kubadilisha sera za kibaguzi za uajiri ndani ya taasisi moja, nao usuluhishi wastani au mkubwa unaweza kutandaa hadi sehemu kubwa ya utumishi kwa umma na sekta ya kibinafsi; na
- mageuzi ya ndani yanaweza kusababisha hatua za ushiriki wa kidemokrasia katika ngazi ya jiji ili kuhimiza ushiriki wa kiraia wa makundi mbalimbali, nazo jitihada za mageuzi ya kitaifa, kikanda au kimataifa zinaweza kushughulikia mada zote kuanzia udhibiti wa mitandao ya kijamii na akiliunde hadi matatizo ya rushwa au ukaidi kama vyanzo vya malalamiko.

Kwa kawaida, mifano hii inagusia tu sehemu ndogo ya vitu vyote vinavyoweza kujumuishwa katika kisanduku cha zana cha kimataifa cha siku zijazo cha mikakati iliyojaribiwa na inayoweza kubadilishwa. Hata hivyo, ili jambo hili lifanyike, ukosefu

wa maafikiano ya kimsingi kuhusu sifa bainifu za utengano lazima hatimaye utatuliwe.

Miongo kadhaa iliyopita, kizuizi sawia kilikuwepo katika tasnia ya utatuzi wa migogoro, wakati zana za uchunguzi zilikuwa chache, mbinu za tahadhari zilikuwa duni, mikakati ya mwitikio ilikuwa ya dharura tu, na hatua za mafanikio zilikuwa za kibaguzi. Leo, kinyume na hili, kuna makubaliano mapana kati ya wasomi na watendaji kuhusu misingi ya utatuzi wa migogoro, hata kama vigezo vyake kamili vinaendelea kujadiliwa na kugeuzwa.

Katika utengano, aina nyingi zinazoendelea za utata kuhusu maswali ya kimsingi inasababisha machafuko fulani katika utendaji na dhana, huku mazungumzo yakizungukia sehemu moja mara kwa mara, yakienda mbali na ushirikiano mkubwa na kupata mafunzo ya kimataifa, badala ya kuyakaribia. Wanaopata hasara ni mifumo ya kijamii na kisiasa ambamo utengano unajikita, na kuleta mchanganyiko wa itikadi kali, migogoro, utofauti na migawanyiko.

## SEHEMU YA TATU: KUWAZIA UWANJA WA UTENGANO

Sehemu hii ya tatu ya makala hii inachunguza kwa ufupi athari – nzuri au mbaya – kuanzisha “uwanja” wa utengano.

Jambo la kwanza linaloonekana ni kwamba vyuo vikuu vikubwa duniani kote vinatoa diploma za nyanja nyingi za masomo – kuanzia anthropolojia hadi uanahabari, migogoro, sayansi ya mazingira, muziki na mipango ya miji. Utengano (bado) haujajumuishwa katika orodha hiyo.

Pili, nyanja ni zaidi ya maeneo ya masomo. Pia zinatumika kama “masoko” ya watendaji ambao hushirikiana au kushindania utambulikaji, rasilimali na kadhalika.

Tatu, katika nyanja zilizokomaa ambapo sekta kubwa ya tatu imeibuka, muda mwingi hutumiwa katika utendaji na utekelezaji suluhu unaodhibitiwa, huku mijadala kuhusu masuala ya kimsingi ikifuata nyuma. Kadiri muda unavyosonga, suluhisho zilizothibitika kufanikiwa katika mataifa mbalimbali mara nyingi huwa sehemu ya ujuzi unaokubalika na unaoweza kuhamishwa kwa uwanja unaohusika.

Hata hivyo, nyanja komavu na zenye wataalamu wengi zinaweza kuambatana na hatua za kirasimu ambapo suluhu za kimfumo hutawala; watendaji wanajishikia nafasi za kitawala; ajenda zinaendeshwa zaidi na wafadhili; utafiti wa kisomi unazuiwa; mafunzo yanazorota kwa sababu ya uradidi; na migawanyo huibuka ambayo hupunguza mafunzo, uratibu na ushirikiano wa tasnia nyinginezo.

Utengano au ukabiliaji wa utengano si uwanja katika fasili yoyote ya kimataifa, kwa hivyo hatua hizi bado hazipatikani sana. Hata hivyo, manufaa haya yameathiri usahihi, mpangilio na muundo wa dhana, mijadala, mikakati na uundaji miungano unaoambatana na uundaji na maendeleo ya uwanja. Kwa hivyo, kuna faida na hasara

zinazopaswa kukadiriwa, hasa na watendaji wenye uwezo na nia makusudi ya kuwekeza katika kiwango cha kimataifa cha kujenga uwanja.

Katika utengano, kuna suala jingine la kukadiria: utawala wa dhana mahususi inayotumika Marekani. Bila shaka, kazi kubwa zaidi ya kitaaluma na shughuli za shirika kuhusu mada ya utengano inatoka Marekani. Hatua hii inaleta faida, kwa mfano, ya kukuzwa kwa maandishi na baadhi ya wasomi na watafiti wakuu wa kimataifa; lakini pia kuna hatari ya tukio linalohusu mtu mmoja, la muda mahususi na mahali mahususi kuanza kuchukuliwa kama aina ya utengano wa kimataifa. Kimataifa, kazi linganishi – na mitandao, miungano na mikutano iliyoandaliwa kwa mtazamo wa kimataifa zaidi – basi itakuwa muhimu.

Kwa sasa, itakuwa hatua muhimu ikiwa, kama makala hii inavyopendekeza, wasomi na watendaji wanaoshughulika zaidi kote duniani watafikia makubaliano ya kimsingi kuhusu hoja (isiyobainika) ya utengano. Manufaa ya kielimu na kiutendaji yatakuwa makubwa sana, bila ya matarajio yoyote ya ukuzaji wa tasnia maalum katika siku zijazo.

## HITIMISHO

Makala hii ya majadiliano imebainisha mfululizo wa utata sugu katika uelewa wetu wa kimataifa wa utengano. Kwa kujibu, makala hii imependekeza fasili ya utengano ambayo, kupitia mjadala wa siku zijazo, unakusudiwa kuendeleza uwezekano wa msingi unaoshirikiwa zaidi kati ya wasomi na watendaji. Ishara ya maendeleo itakuwa kupunguza polepole wingi wa vivumishi vya sifa ambavyo vinatumika sasa, ambavyo vimesababisha mkanganyiko zaidi kuliko uwazi. Hatimaye, itawezekana kuzungumza kuhusu utengano kwa ufasaha unaotumika kurejelea ufarakano.

Makala hii, ikikopa kutoka utafiti wa kimataifa, na kazi ya IFIT yenyewe, imeanzisha wigo elekezi wa suluhisho la utengano ambalo linaendana kwa mapana na fasili iliyopendekezwa. Wigo huo unaangazia kwamba hatua za kukabiliana na utengano ni pana mno, na zinatoa vigezo vya muundo wa usuluhishi kulingana na muktadha unaohusika.

Hata hivyo, suluhisho litawavutia wale tu wanaochukulia utengano kuwa tatizo kubwa; ambalo hakuna jamii au mfumo wa kisiasa unaweza kujitakia. Kuhusu hili, bado kuna watu wengi wanaotilia shaka – watu ambao, kwa mfano, wanachukulia utengano kuwa upotoshaji au ukengeushaji unaosababisha upuuzaji wa masuala au maovu muhimu zaidi ya kijamii; kama hoja ya kiusemi tu au kisingizio cha walio wengi cha kulazimisha maafikiano ya kisiasa yasiyokubalika au mipangilio ya kudumisha hali ilivyo dhidi ya makundi ya wanyonge; kama neno la kuwazuia wanaharakati kutumia mbinu za kukabiliana au kugawanya zaidi; au kama suala ambalo hatari zake halisi zimetiliwa chumvi.

Mashaka hayo yanakubaliwa na kueleweka. Hata hivyo, kwa sababu mashaka haya yanaweza kujengwa juu ya uelewa tofauti sana wa utengano, makala hii inatoa mwito wa kurudi nyuma hatua moja ili kufafanua kanuni za kwanza kwa udhahiri

zaidi. Jambo hili likitokea, tunaweza kugundua kile kinachoshuhudiwa katika kazi ya kimataifa ya IFIT katika mataifa mbalimbali ya kimabavu, dhaifu na yaliyoathiriwa na mizozo: aina zote za utengano ni jambo linalopaswa kuepukwa. “Kwa nini hatukuchukua hatua mapema?” ni swali ambalo tunapaswa kuepuka wakati ujao.

**Shukrani**

Mwandishi angependa kuwashukuru wafanyakazi wenza, washirika na wataalamu waliochangia maarifa muhimu katika mikutano, makongamano na warsha mbalimbali zilizofanywa na IFIT pamoja na Ford Foundation katika mwaka uliotangulia chini ya ufadhili wa Mpango wa Kimataifa wa Kukabiliana na Utengano. Maarifa haya yamechangia mawazo muhimu na hoja zinazoendelezwa katika makala hii. Mwandishi pia anatoa shukrani maalum kwa Hilary Pennington, Annamie Paul, Barney Afako, Dana Habib, Alejandra González, Jasmina Brankovic na Melanie Greenberg kwa maoni yao bora na matoleo ya awali ya jarida hii.

**Kuhusu IFIT.** Taasisi ya “Institute for Integrated Transitions” (IFIT) iliyoanzishwa mnamo mwaka 2012, ni shirika huru, la kimataifa, lisilo la kiserikali linalotoa uchanganuzi wa taaluma mbalimbali na usaidizi wa kiufundi kwa wahusika wa kitaifa wanaoshiriki katika mazungumzo na mabadiliko katika mataifa tete na yaliyoathiriwa na migogoro. IFIT imeunga mkono mazungumzo na mabadiliko katika nchi mbalimbali zikiwemo Afghanistan, Kolombia, El Salvador, Libya, Meksiko, Naijeria, Sri Lanka, Sudan, Siria, Gambia, Tunisia, Ukreni, Uzbekistan, Venezuela na Zimbabwe.